SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.17Decembre 2025

# UTAMADUNI WA AFRIKA UNAVYOTAMBULISHA MAADILI NA THAMANI YA FASIHI YA KISWAHILI

**Simba Haji Gora**
simbagora0@gmail.com
**Dkr. Athumani Salum Ponera**
**Dkr. Masoud Nassor Mohamed2**
School of Swahili and Foreign Languages,
Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA

*Received: Augest 2025, Accepted: October 2025, published: Decemer 2025*
*© SUMAIT University Journal 20225*

**Abstract**
*This article has examined the moral tensions in Swahili films and how they highlight the value of Swahili literature. To achieve this goal, the article has analyzed moral conflicts in two main areas. First, beliefs concerning Swahili customs. In this section, it has been revealed that there exists a tension between preserving Swahili traditions and norms, the importance of premarital education, and differing views on tradition versus modernity. Second, the study has analyzed philosophical conflicts. In explaining these philosophical tensions, the article has explored beliefs about circumcision and initiation among the Swahili, the role of reproduction and child upbringing, and beliefs about death. Data collection and analysis were conducted through the textual review method and analyzed thematically by observing and examining Swahili films. The analysis was guided by the theory of axiology, specifically its branch dealing with ethics.*

**Ikisiri:**

*Makala hii imechunguza mvutano wa kimaadili katika filamu za Kiswahili na namna unavyoibua thamani ya fasihi ya Kiswahili. Katika kufikia lengo hilo makala hii imechambua mivutano ya kimaadili katika maeneo makuu mawili. Mosi, imani juu ya desturi za Mswahili. Katika kipengele hiki kumebainika kuwapo kwa mvutano katika kulinda mila na silka za Mswahili, umuhimu wa mafunzo ya ndoa na mitazamo kuhusu ukale na usasa. Pili, kumechambuliwa mivutano kuhusu falsafa. Katika ufafanuzi wa mivutano ya kifalsafa kumechambuliwa imani juu ya mkole na jando kwa Waswahili, nafasi ya uzazi na malezi ya mtoto na imani kuhusu kifo. Ukusanyaji na uchambuzi data umefanywa kupitia mbinu ya udurusu matini na kuchambuliwa kwa mbinu ya kimaudhui kwa kuzitazama na kuzichambua filamu za Kiswahili. Uchambuzi huo umehusisha nadharia ya aksiolojia kwenye tawi na maadili.*

Keywords: **Utamaduni wa Mswahili, Filamu za Kiswahili, Mvutano, Aksiolojia, Thamani ya Fasihi**

## 1.0 UTANGULIZI

Thamani ya fasihi inafafanuliwa kwa mitazamo tofauti kutegemea mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Mitazamo hiyo inaweza kujitofautisha kati ya kundi moja na jingine. Kwa mfano, [10] anaigawa thamani ya fasihi kwa kutumia mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni ule wa kimajumui. Mtazamo huu unatazama usanii uliomo ndani ya kazi ya sanaa kwa jicho la mvuto wa sanaa husika kwa kutumia lugha teule na yenye kutoa burudani kwa msomaji. Pili, fasihi inaweza kuwa na thamani ya kiujumi. Msanii anapoweza kuwasilisha ujumbe kwa kutumia njia mbalimbali kuilenga jamii. Hapo msanii huyo huonekana amefanikiwa kuonesha thamani ya fasihi. Akiendelea kutoa ufafanuzi wake [10] anaeleza , ni wazi kuwa fasihi hupimwa kwa kipimo cha kithamani kutokana na namna ya uwasilishaji wake au katika ujumbe uliomo kwenye kazi inayohusika. Ingawa maelezo yake ni ya kinadharia tu lakini yanatanabahisha kuwa, thamani ya fasihi ni jambo la msingi ndani ya fasihi.

Kwa upande wa [4] anazungumzia mitazamo ya wahakiki na waandishi wa kazi za fasihi katika msisitizo wa thamani ya fasihi kwa jamii. Anasisitiza kwa kusema, wahakiki wengi wa fasihi hawazingatii kuhusu umuhimu wa thamani katika fasihi. Katika maelezo yake, anaonesha jinsi thamani ya fasihi inavyoweza kuhusiana moja kwa moja na fasihi yenyewe. Pia thamani hiyo inaweza kuhusishwa na maadili ya jamii. Uzoefu wa uzuri na ubaya katika fasihi nao unaweza kutazamwa kama thamani ya fasihi. Thamani ya fasihi ni suala lililojadiliwa kwa muda mrefu na kusababisha kuwapo kwa mitazamo tofauti kutoka kwa wanafalsafa mbalimbali. Maelezo ya [4]. katika kuitazama thamani ya fasihi yameonesha namna waandishi wanavyosisitiza thamani ya fasihi kama inavyoonekana katika kazi za kifasihi.

Kupitia maelezo yake tumejifunza kuwa msisitizo wa thamani katika jamii ni jambo la msingi sana. Pamoja na maelezo hayo, bado hakutazama ni thamani ipi inapaswa kuwapo katika fasihi ya jamii fulani. Pia, hakuonesha ni kwa vipi thamani hiyo huwa inaibuliwa. Kwa hivyo, utafiti uliofanyika umegundua ulazima wa kuwapo kwa thamani katika fasihi na ndiyo maana ukanuwia kuchunguza nafasi ya mvutano wa kimaadili katika kuibua thamani ya fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wataalamu wa fasihi wanasisitiza kuwa fasihi ni lazima iwe na thamani yake kutegemeana na jamii.

Pia, ufafanuzi wa [9] unabainisha thamani ya ujumi wa Kiafrika katika vipengele kadhaa, ambavyo ndivyo vinatambulisha na kuathiri utamaduni na maisha ya Waafrika kwa sehemu kubwa. Vipengele hivyo vya kiujumi huambatana na umbo la ndani la kazi ya fasihi. Vipengele anavyovijadili [9] katika makala yake ni kuishi kwa ushirika, utu, utii na adabu, makusudio, ushababi, ukizinda, na imani za dini. Anaonesha kuwa, kuishi kwa ushirika ni miongoni mwa vipengele vya kithamani vilivyoelezwa na waandishi wa hadithi fupi. [9] anasisitiza kuwa, mifumo iliyoundwa na watu kwa ajili ya kuiongoza jamii ikijadiliwa na waandishi wa fasihi huwa inalenga kuona kuwa, fasihi hiyo inayo thamani ya kijamii.

Maelezo hayo ni muhimu kwa sababu yanaonesha wazi kuwa kila utanzu wa fasihi unaweza kuwa na thamani yake. Vilevile, yamebainisha kwa uwazi thamani za kifasihi zinazopatikana katika kazi ya fasihi kwa kuiona jamii huwa ndio mwanzilishi, mwangalizi na mwelekezaji wa mienendo na

masuala mbalimbali yanayopaswa kuwemo katika fasihi. Pia, mwanafasihi ndiye anayesadifu mfumo wa jamii kwa kuunasibisha na imani kwa Miungu. Matakwa ya imani za dini kuhusu himizo la kufanya matambiko, miviga, ibada na sherehe kiushirika ni ushahidi kuwa mfumo huu una mizizi katika masuala ya kiimani. Hivyo, Waafrika walisisitiza maisha ya ushirika kama kanuni ya msingi ya maisha. Hivyo basi, fasihi yoyote yenye misingi hiyo huwa ina thamani. Kwa maana hiyo, utafiti uliofanyika umeona ipo sababu ya kuangalia mvutano wa kimaadili katika kuimarisha thamani ya fasihi ya Kiswahili kwa kujiegemeza katika filamu za Kiswahili. Ingawa [9] ameonesha namna fasihi inavyobeba thamani, lakini hakuonesha kuwa thamani hiyo inajengwa na mambo gani, ndiyo maana utafiti uliofanyika ukaamua kuchunguza nafasi ya mvutano wa kimaadili katika kujenga thamani ya fasihi ya Kiswahili.

[3] wanafafanua thamani ya fasihi kwa kuigawa katika makundi kadhaa. Mosi thamani ya kisiasa: Katika thamani hii anaona kuwa kazi ya fasihi inaweza kumsukuma mtu kuchukua hatua inayoweza kufichua dhuluma, kutoa sauti kwa wanaoonewa, kuwadhihaki mafisadi, na ikawa inajaribu kuwashawishi watu kuanza kutenda na kufikiria kwa njia yenye tija kwao. Pili, anafafanua thamani ya kitamaduni. Ikiwa kazi inashughulikia mitazamo, desturi, na maadili ya wakati wao au wakati mwingine, kazi hiyo hutazamwa kuwa na thamani ya kitamaduni. Tatu, anafafanua thamani ya kifalsafa kwa kujumuisha fasihi yenye kuchunguza kwa undani kuwapo kwa kitu, au maumbile na namna kinavyofanya kazi. Kazi ikijipambanua kwa mitindo hiyo huhesabiwa kuwa kazi hiyo ina thamani. Hivyo, filamu nayo inaweza kuchunguzwa kwa mtindo wa kithamani na kimaadili kama zilivyo tanzu nyingine kwa sababu filamu ni aina mojawapo ya sanaa yenye umaarufu zaidi katika ulimwengu huu wa utandawazi.

[7] anafafanua kwa kueleza kuwa , thamani ya fasihi ni jambo lisiloepukika katika fasihi. Jambo hilo linakutana na kanuni zinazojulikana za uhakiki wa fasihi. Thamani hiyo inatokana na kuchunguza ujuzi alionao mwandishi, lengo la kazi, upekee wa ubunifu, uasili wa kazi za sanaa, athari ya masimulizi, kuishi katika nyakati zote, ubunifu unaotambulisha utamaduni wa kijamii, ubunifu unaotegemea soko, na kuchunguza tabaka lengwa. Maelezo ya [7] yanaweka vigezo msingi katika kuchunguza thamani ya fasihi. Vigezo hivi vinatoa nafasi ya kuona kuwa, fasihi haiwezi kujikamilisha yenyewe bila ya kuwa na thamani. Mawazo haya yana mchango muhimu katika utafiti uliofanyika kutokana na kuonesha kuwa, thamani katika fasihi ni jambo muhimu na hutazamwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Hivyo, uchunguzi wa mvutano wa kimaadili katika kuibua thamani ya fasihi umetazamwa katika makala hii kama vipengele anuai vya filamu teule.

Kwa ujumla, maandiko hayo yameacha mapengo yafuatayo: Mosi, hayajaonesha mvutano wa maadili ya jamii tofauti katika filamu, na fasihi kwa jumla. Pili, hayajabainisha thamani inayopatikana kutokana na mwingiliano au mvutano wa maadili hayo. Kutobainishwa kwa masuala hayo kumeonesha hali ya kutomakiniwa kwa maadili ya kijamii katika kazi za fasihi na kuonekana hakuna thamani yoyote inayotokana na mvutano wa kimaadili uliopo katika kazi za fasihi. Kwa kuzingatia hali hiyo, ndiyo maana mtafiti akachunguza utamaduni wa muafrika unavyochochea mvutano wa kimaadili katika kuibua thamani ya fasihi ya Kiswahili kupitia filamu teule.

## 2.0 Methodolojia na Nadharia

Makala hii imetumia mbinu ya uchanganuzi matini katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii inahusika katika upitiaji wa nyaraka, vitabu, kusikiliza sauti katika vyombo vya kunasia sauti au kuangalia video. Data za utafiti wa makala hii zilikusanywa kwa kuangalia filamu teule kwa umakini na kuchuja dondoo zilikwenda sambamba na malengo ya utafiti. Aidha, mkabala wa kimaelezo ulitumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data. Kwa vile utafiti wa makala hii ulichunguza filamu, njia hii imetumika na imefaa sana katika kukusanya data. Mtafiti amechambua kwa makini filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu* ili kugundua taarifa za msingi katika filamu hizo. Aidha, nadharia ya aksiolojia imetumika katika uchanganuzi wa taarifa za makala hii kwa kuzingatia tawi la kimaadili. Tawi la kimadili linahusika na uainishaji wa maadili kwa kuchunguza kipi au lipi ni sahihi na kinyume chake. Aksiolojia ni nadharia inayojihusisha na nyanja nyingine mbalimbali za kifalsafa ambazo hutegemea sana dhana ya thamani, kama vile ujumi au falsafa za kidini. Kwa ujumla Aksiolojia ni nadharia ya thamani na maadili na imetumika kukusanyana kuchambua data za makala hii.

## 3.0 VIPENGELE VYA KITAMADUNI VINAVYOCHOCHEA MVUTANO WA KIMAADILI

Utafiti wa makala hii umebaini kuwapo kwa vipengele vinavyoibua mvutano wa kimaadili. Vipengele ambayo huibua thamani ya fasihi kwa mujibu wa jamii ya Waswahili. Vipengele vilivyobainika ni imani juu ya desturi za Mswahili. Katika kipengele hiki kumechambuliwa imani juu ya deturi za Mswahili na mvutano katika kulinda mila na silka za Mswahili na mitazamo kuhusu ukale na usasa. Pia kumebainika kipengele cha falsafa ya kiafrika. Kipengele hiki kimejengwa na imani kuhusu mkole. Nafasi ya uzazi na imani kuhusu kifo. Ufafanuzi wa vipengele hivyo ni:

### 3.1 IMANI KATIKA DESTURI ZA MSWAHILI

Imani na desturi za jamii ni nguzo kuu zinazounda utamaduni na utambulisho wa watu ndani ya jamii fulani. Imani ni mitazamo na dhana ambazo jamii huamini kuwa ni sahihi kuhusu maisha, uhusiano wa binadamu, na ulimwengu unaowazunguka, ikiwemo mambo ya kiroho, kidini, na kijamii. Kwa upande mwingine, desturi ni mwenendo wa maisha unaoonesha jinsi jamii inavyotekeleza imani zake kupitia vitendo kama sherehe za kifamilia, ndoa, mavazi, malezi, na namna ya kuhusiana kijamii. Kupitia imani na desturi, jamii huweza kudumisha maadili, mshikamano, na heshima baina ya wanajamii, huku zikiwa urithi muhimu unaotambulisha asili na falsafa yao ya Maisha. Waswahili ni kundi la kijamii linalomiliki mila na silka zake. Hivyo, sehemu hii inafafanua imani hizo kupitia mvutano wa kulinda mila na silka za Mswahili, umuhimu wa mafunzo ya ndoa, na mitazamo kuhusu ukale na usasa.

#### 3.1.1 Mvutano katika Kulinda Mila na Silka za Mswahili

Nguvu ya kulinda silka na mila za Mswahili ni miongoni mwa sababu zilizoibua mvutano wa kimaadili. Hii imesababisha mtunzi kutumia mitindo ya mvutano wa kimaadili katika filamu zake. Maadili ya Mswahili ni jumla ya kanuni na utaratibu unaothaminiwa zaidi na watu wa asili ya Pwani ya Afrika Mashariki pamoja na kuenea katika bara zima la Afrika. Hivyo, mtunzi wa filamu

hizi ametumia maadili hayo ili kupingana na filamu za Waswahili zinazotumia maadili ya nje. Maadili yanayohimizwa na mtunzi yanajumuisha mila na silka za Waafrika.

Mtunzi wa filamu ya *Matusi* anaonesha kuwa mila na silka ni utashi unaopaswa kuzingatiwa na kila Mswahili. Ushahidi wa hayo unathibitishwa na mazungumzo ya mhusika Kutafuna na Bashite, kama inavyodokezwa katika data ifuatayo:

**Kutafuna:** Unajua nyinyi wanaume wa Dar es Salaam ukiacha jinsia, tofauti yenu na dada zenu ni ndogo.

**Bashite**: Kwa nini?

**Kutafuna:** Utamkuta mwanamme anajipaka *perfume* na anamiliki kioo sababu ya kujichubua. Mbaya zaidi, unaweza kumkuta mwanamme anajichora michoro ambayo kwetu tunamchora bi harusi.

**Bashite**: Inaonekana mjomba hujui chochote kuhusu mambo ya kisasa.

**Kutafuna:** Ndio, huku kwetu kuna mila, Dar es Salaam kuna mitandao. Halafu usichokijua mjomba, uhuru wetu hauwezi kuwa na maana kama tutaendelea kuacha utamaduni ukiteketea.

**Chanzo**: *Matusi,* onesho la 3, dakika ya 2:14 hadi 3:41

Katika muktadha wa mazungumzo haya kati ya Kutafuna na Bashite, dhana ya mila na silka inaweza kuchambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Aksiolojia ili kuelewa mgongano wa maadili kati ya utamaduni na mabadiliko ya kisasa. Nadharia ya Aksiolojia inahusu masuala ya maadili na thamani, ikichunguza kitu kinachothaminiwa katika jamii fulani, na jinsi maadili yanavyoathiri tabia na uchaguzi wa mtu binafsi au jamii. Katika nukuu hiyo, Kutafuna anaonekana kushikilia maadili ya Mswahili kwa dhati, akionesha msimamo kwamba, mila na silka ni sehemu muhimu za utambulisho wa mtu na jamii. Katika mazungumzo, anasema, "huku kwetu kuna mila" akionesha kuwa mila zao zinathaminiwa sana. Thamani ya mila inahusiana na uhifadhi wa utamaduni wa asili, ambapo kuna msisitizo wa kuheshimu maadili yanayoweka mipaka ya tabia na mwonekano wa kijamii wa wanaume na wanawake. Kutafuna anapinga mienendo ya kijamii ambayo inakwenda kinyume na mila, kama vile wanaume kujipaka manukato na kujichora, akifananisha tabia hizi na "bi harusi".

Maelezo ya Kutafuna kuwa “uhuru wetu hauwezi kuwa na maana kama tutaendelea kuacha utamaduni ukiteketea” yanaendana moja kwa moja na msingi wa nadharia ya Aksiolojia inayoeleza kuwa mila na silka ni vitu vyenye thamani ya juu vinavyopaswa kuhifadhiwa ili kulinda utambulisho wa jamii na uhuru wa kweli wa watu.

Kwa upande wa mhusika Bashite, tunapata mwelekeo tofauti wa kimaadili. Bashite anawakilisha kizazi kipya au wale wanaothamini mambo ya kisasa na mabadiliko ya kijamii. Bashite Amechorwa kitaswira kuonesha tabia ya wale wanaokataa mila na silka za jamii. Hayo yanajidhihirisha pale anaposema: "inaonekana mjomba hujui chochote kuhusu mambo ya kisasa." Anaonesha thamani ya mabadiliko ya kiteknolojia na kijamii, kama vile matumizi ya mitandao na mtindo wa kisasa wa

maisha. Hii ndio sababu ya mvutano wa kimaadili. Fikra hii inatokana na msingi wa nadharia ya Aksiolojia unaofafanua kuwa, fasihi inapaswa kuthaminiwa kwa uzuri wake wa asili bila ya kuathiriwa na mhemko. Hivyo, msisitizo wa maadili ya Mswahili katika filamu hii ni ishara ya kuibakisha sanaa ya filamu kwenye uzuri wake wa asili.

### 3.1.2 Umuhimu wa mafunzo ya ndoa

Eneo jengine linaloonesha hamu ya kihifadhi mila na silka za Mswahili ni maelezo ya Babu kwa mjukuu wake (Bashite) wakati akimueleza umuhimu wa kupewa mafunzo ya jinsia wakati wa baleghe. Babu anaona kuna umuhimu wa Mswahili kufundishwa mambo yote yanayohusu mila na silka za jamii yake kwa sababu ameshaathiriwa na mila za kizungu. Aidha, kufuatwa kwa mila za kizungu kunahesabiwa sio mapungufu bali ni kukosa adabu. Maelezo hayo yanathibitishwa na mazungumzo ya mhusika Babu na mjukuu wake (Bashite) waliposema:

**Babu**: Mimi nimekuelewa sana lakini yule ni kiongozi wa ukoo huu, lakini mjomba wako anayafanya ili wewe usipate tabu, maana wewe ulitakiwa uje huku kipindi cha baleghe, ila uzungu uliupa nafasi na ndiyo maana leo ukaleta mzungu hapa.

**Bashite**: Yule sio mzungu babu, ila anatabia ambazo hazimridhishi mtu wa huku, halafu mimi sioni sababu ya mjomba kutotoa Baraka zake, eti mpaka afundishwe, wakati huenda mapungufu yake ndio sababu ya kumpenda.

**Babu**: Bashite, kwetu kuna mila na katika mila
kuna miiko, kumbuka tamaduni haijaacha kitu… kweli mapungufu yapo lakini kukosa adabu sio mapungufu.

**Chanzo**: *Matusi*, onesho la 3, dakika 09:51 hadi 10:29

Nukuu hii inaonesha wazi kuwa sababu ya mgogoro wa kimaadili ni imani juu ya mila na desturi za kijamii. Mswahili anaona kufuata mila za jamii yoyote pamoja na usasa ni jambo la kawaida na lisilo na madhara yoyote. Kwa upande wake, Babu anahimiza maadili ya Waswahili na jadi zao.

Eneo jingine linaloonesha nguvu ya kupigania mila na silka za Mswahili ni pale Mswahili alipolalamikia maneno anayoambiwa yeye pamoja na mchumba wake. Mazungumzo yao ni haya:

**Bashite:** Yale maneno yamemtia unyonge mpenzi wangu.

**Mjomba**: Unajua, wakati mwingine inahitajika giza ili uone vizuri, Ulichokosea wewe ni kumchukua yule mwanamke mjini na kumleta huku. Ilikuwa umtoe Dar es Salamu na umpeleke Ulaya kwa sababu wanawake wengi wa Dar es Salaam wanaamini baba wa wanaume zao wanaishi Ulaya. Na hii inatokana na nyinyi wenyewe kuishi sana Kimarekani na kuthamini vilika vya uhaibuni kuliko vya asili yenu.

**Kutafunwa:** Bado sijakuelewa

**Mjomba:** Kizazi chenu kimekosa heshima ya kujiheshimu na kuliheshimu taifa na tamaduni kwa ujumla. Twaweza kusema, nyinyi ndio chanzo cha heshima za wasichana mliokuwa nao.
**Kutafuna:** Lakini mapungufu ni sehemu ya ubinaadamu.
**Mjomba:** Ni kweli, lakini kukosa adabu sio mapungufu, bali ni matokeo ya mzazi au mwalimu aliyemfundisha.
(**Chanzo**: *Matusi,* onesho la 1, dakika 10:05 hadi 11:06)

Kwa mujibu wa maelezo hayo, ni wazi kuwa sababu iliyochochea mvutano wa kimaadili ni nguvu ya kupigania ustawi wa mila na silka za kijamii. Hivyo, tawi la maadili lililopo katika nadharia ya Aksiolojia pale mjomba aliposema ‘ulichokosea wewe ulikuwa umtoe Dar es Salamu na kumpeleka Ulaya linaonesha kutokubalika kwa matendo ya mchumba wa Bashite.

Katika mazungumzo ya Mjomba na Kutafuna, mvutano wa kimaadili unaonekana kwa sababu pande mbili zinabishania masuala ya uwajibikaji wa kimaadili kwa heshima na adabu katika jamii. Mjomba anaamini kuwa kizazi cha vijana kimekosa heshima kwa mujibu wa msingi ya kitamaduni. Kwa mujibu wa Kutafuna, mapungufu ya kimaadili si sehemu ya ubinadamu bali ni kukosa heshima.

Kwa upande wa filamu ya *Wali Wangu*, mtazamo kuhusu silka na mila za Waswahili unapewa umuhimu mkubwa. Lengo ni kuhamasisha elimu isiyo ya mkondo rasmi kuweza kuwasaidia wanajamii katika maisha yao. Hata hivyo, mvutano juu ya jambo hili umekuwa mkubwa. Mvutano huo unasababishwa na mabadiliko ya wakati. Katika filamu hii, mhusika Mwalimu anaonesha umuhimu wa kuwafunda wanawake kabla hawajaingia katika ndoa au hawajashiriki matendo ya ngono. Mila za Kiafrika zinaruhusu utoaji wa elimu hiyo kama anavyofafanua mwalimu:

**Mwalimu:** …Na msipomfunda kipindi cha usichana wake, tatizo litakuwa kubwa atakapotaka kuwa mwanamke. Lakini akiwa mwanamke kipindi mshamaliza yenu nahakika hatawalaumu.
**Mama Shata**: Kisado aliniambia kuwa ulikaa naye.
**Mwalimu:** Ndio lakini kilichokomaa kukiondoa katika ukomavu wake inahitajika subira…ila nyakati zinaharibu mambo
Chanzo: *Wali Wangu,* onesho la 4, dakika ya 4:12 hadi 5:00

Nukuu hii ni tanbihi ya mwalimu juu ya Shata kupewa mafunzo yanayohusu usichana wake kabla ya kuwa mwanamke. Maelezo hayo yanaonesha mvutano wa muda kwa namna mbili. Mosi, mabadiliko ya teknolojia yanaweza kuathiri mno mila na desturi za jamii. Pili, kucheleweshwa kwa Shata kupatiwa elimu ya ujinsia na ngono salama ndio kumesababisha Shata kujiingiza kwenye ngono. Aidha, muda wa kutaka kumfunda unaonekana umeanza kutoweka, ndiyo maana mwalimu anatanabahisha kuwa kukiondoa kilichokomaa katika ukomavu wake inahitaji subira. Hii inaashiria kuwa Shata ameshakuwa mzoefu kwenye uzinzi. Hivyo, inahitajika juhudi kubwa ili kumfanya aache tabia hiyo.

**[8]** anaunga mkono kuhusu elimu ya Waafrika kabla ya kuja kwa ukoloni. Anaeleza kuwa, Bara la Afrika lilikuwa na taasisi zinazosimamia ujuzi na mafunzo kabla ya kutawaliwa na ukoloni na hata

kabla kuwasili kwa wamisionari. Mifumo ya mafunzo ya Waafrika kama vile shule za jadi ilikuwapo, lakini taasisi muhimu zaidi ni kitengo cha familia ambacho kilitumika kwa utoaji wa maarifa na upataji wa ujuzi na elimu. Hata hivyo, taasisi hizi hizi za mafunzo zilidhoofishwa kutokana na kuingizwa na kulazimishwa mifumo ya maarifa kutoka kwa nguvu za kikoloni.

### 3.1.3 Mitazamo Kuhusu Ukale na Usasa

katika kulinda maadili na silka za Mswahili, mtunzi wa filamu hizi anaikabili mitazamo kuhusu ukale na usasa. Katika filamu ya *Matusi*, kipengele cha mvutano wa kimaadili kinachorwa katika mtazamo huu kwa kuonesha umuhimu wa kulinda mila na silka katika nyanja zote za maisha. Miongoni mwa mambo yanayosisitizwa yanahusu matumizi ya zana za kale katika ustawi wa maisha ya watu. Ushahidi wa hilo unapatikana katika wimbo ufuatao:

> Mwanangu kua uyaone ya dunia ilipofikia na inapoelekea
> Usiyaonee muhali ndani tukayagubika, tunazo kila dalili kumbukumbu kuziweka
> Aaaaa, Wanawake wa mjini wameacha asili zetu,
> Waendekeza uhuni kufuata mila za watu
> Wanawake wa kileo aaaaaaa,
> Wameacha mila zao aaaaaa
> Wanaiga kwa wenzao, oooooooh
> Wameacha mila za kwao, oooooooh
> Waendekeza uhuni eeeeeee
> Kizazi ndipo hufeli na maadili kuporomoka
> Kwa kujiona tayari usukani tumeshika
> Vyema tuelewe hili vifaa vilitumika,
> Mchi, kinu kiukweli majumbani tuliweka
> Karabai na kandili vyetezo vilitumika vyema tuelewe hili vifaa vilitumika.
> **Chanzo**: (*Matusi,* onesho la 8, dakika 7:10 hadi 8: 02)

Nukuu hiyo inaonesha namna vijana au jamii inavyodharau mila na utamaduni wa Mswahili. Kwa upande mwingine, nukuu hiyo inataja baadhi ya vitu vya asili kama vile, karabai, kandili, chetezo, kinu na mchi kwa msisitizo wa kuendelea kuvitumia vitu hivyo. Vitu vyenye asili ya Mswahili vinapaswa kutunzwa na kuenziwa hata kama kuna mabadiliko ya teknolojia. Wimbo huo unaonesha wasiwasi wa mtunzi kuhusu mabadiliko ya kijamii, hasa tabia na maadili ya wanawake wa mjini. Kwa kutumia Nadharia ya Aksiolojia, jamii inaweza kufasiri mabadiliko haya kwa njia ya kulinganisha thamani za kitamaduni na za kisasa.

Kwa mujibu wa misingi ya Nadharia ya Aksiolojia, kupitia tawi la thamani, ukale huwa na thamani ya Juu. Kipande cha wimbo kinachosema, "Wanawake wa mjini wameacha asili zetu, waendekeza uhuni kufuata mila za watu" kinaonyesha kuwa mwandishi anapinga usasa ambao unaleta mabadiliko yanayochukuliwa kuwa hasi, kama kuiga tamaduni za kigeni na kuacha maadili ya jamii. Hii inawakilisha kutetewa kwa thamani za kitamaduni (ukale) kama mwongozo wa kuishi kwa maadili mema.

Aidha, kupitia wimbo huo, Nadharia ya Aksiolojia inafasiri usasa kwa kuupa thamani ya chini. Kauli kama "wanaiga kwa wenzao, na kuacha mila za kwao" inaashiria kwamba kuiga utamaduni wa kigeni kunaonekana kama kuporomoka kwa maadili na kupoteza utambulisho wa kitamaduni. Usasa unachukuliwa kuwa na thamani ndogo, kwa sababu unavunja duara la maadili na tabia za kale zinazochukuliwa kuwa msingi wa uadilifu. Kwa mujibu wa wimbo huo, matokeo ya kuporomoka kwa maadili yanatazamiwa kwamba kizazi kinaweza kufeli na maadili kuporomoka kwa sababu ya kupoteza mwelekeo wa kitamaduni. Katika mshororo usema "Kizazi ndipo hufeli na maadili kuporomoka" ni ishara ya onyo kuhusu thamani ya kijamii ya kuzingatia maadili ya kale ili kuzuia madhara ya kimaadili kwa vizazi vijavyo.

Pia, wimbo huo unafafanua umuhimu na thamani za kazi na zana za nyumbani. Vifaa vya asili vilivyotumika nyumbani kama vile "mchi, kinu, karabai na kandili" vinapewa umuhimu kama ishara za maisha ya kitamaduni yenye thamani. Mabadiliko katika matumizi ya vifaa hivyo yanaweza kuchukuliwa kama dalili ya kuporomoka kwa thamani ya kazi za nyumbani, jambo linasababisha mvutano kati ya usasa na kale.

Maelezo hayo yanaonesha kuwa jamii imebaki katika njia panda juu ya maadili na teknolojia; ndiyo maana mtunzi wa filamu hii akaonesha uhalisi uliopo katika jamii zetu za Kiafrika. Kwamba, vijana wengi wanakumbwa na uleo au usasa na kudharau maadili ya jamii. Fikra hii inasisitizwa na Chanuo Mtanzania (2023)[1]. Anasema:

> Sababu mojawapo ya kuiita "*Matusi*" ni kuonesha namna tunavyoweza kuyakabili mabadiliko katika nyanja za utamaduni. Wapo watendao '*Matusi'* kwa kudharau silka na desturi zetu. Sayansi na teknolojia imeshawateka watoto wa kishuwa ambapo huwa hawatilii shaka juu ya kuendeleza maadili yetu. Hata Mswahili ni mtoto wa kishua; tulimchukua kutoka Osterb na maigizo yake yenye kuonesha utamaduni wa Kiulaya na kumleta huku 'uswazi' ili aone mazingira halisi ya Mtanzania.

Dondoo hili linaonesha kuwapo kwa makundi mawili makuu ya uigizaji wa filamu. Kundi la kwanza ni la watoto wa kishua ambalo hutunga filamu zao kwa kutumia majengo makubwa ya roshani, kukodi magari na maofisi ili kuonesha maisha ya hadhi ya juu kuliko uhalisia wa maisha yao. Kundi hili huwakilisha mila silka na desturi za ughaibuni na ndiyo maana kusema hazifuati maadili ya Waswahili. Kundi la pili ni la watoto wa *kiswazi* ambao huwa na maisha ya kawaida, yasiyo mbwembwe nyingi za kimaisha. Hivyo, uigizaji wa watoto wa uswazi unaonekana hutawaliwa na mambo yanayoigusa jamii moja kwa moja na kulinda mila na silka za jamii.

Kwa upande wa filamu ya *Wali Wangu*, dhana ya ukale na usasa inatazamwa kwa mtazamo wa mila na desturi zinazofaa kuendelezwa katika jamii. Pia, zinazopaswa kupingwa na kupigwa marufuku katika jamii. Mila zinazokubaliwa ni ngoma za jadi na kuwacheza wanawari. Ushahidi wa hili unaonekana mwisho wa onesho la saba na mwanzo wa onesho la nane, kutoka dakika 02: 00 hadi

---

[1] Maelezo haya yalitolewa na Chanuo, ambaye ni "producer" na mwigizaji wa filamu hii wakati akihojiwa na chaneli ya mtandaoni inayoitwa "studio 9 entertainment". Mtafiti ametazama mahojiano hayo *Youtube* tarehe 14/11/2024.

03:35. Katika tukio hilo, kunatokea mvutano wa maadili kuhusu kumtoa mwari kupitia ngoma hiyo. Mvutano huo unatokea baada ya wazee wa Shata kumtoa mwari bila ya taarifa kwa wale waliopeleka barua ya posa. Hali hiyo inajidhihirisha kwa mazungumzo ya Katambuga aliposema:

**Katambuga:** Hivi nikiamua kufanya fujo ntaonekana mkorofi

**Mwalimu:** Kwa nini Katambuga ufanye fujo?

**Katambuga:** Kwa nini wanamtoa mwari wakati majibu hawajarudisha, nilifanya jambo la busara kupeleka barua sasa wao wanatoa maamuzi bila kushauriana, kweli?

**Mwalimu:** Yule ni mtoto wao wanayo mamlaka, hebu kuwa mvumilivu pengine wanakamilisha hili kisha watakupa majibu.

**Chanzo**: *Wali Wangu*, onesho la 8, dakika ya 03: 06 hadi 3:52

Nukuu hii inafafanua eneo jingine linaloonekana kufuata jadi. Wahusika katika filamu ya *Wali Wangu* wanakamilisha ada za kijamii kama vile kumfunda mwari, na kuwekwa utawa kwa mwanamke anayeolewa pamoja na kuwapo kwa ngoma za harusi. Hata hivyo, mvutano wa kimaadili unaibuka baada ya Kambaulaya kutopewa majibu ya barua yake ya posa.

Mbali na mtunzi kushikilia ukale na kuendeleza jadi za jamii, bado wataalamu wanaona hatupaswi kudharau moja kwa moja maendeleo na mabadiliko ya leo kutokana na tija zake**.** [1] ameonesha madhara pamoja na jitihada zinazochukuliwa katika kukabiliana na usasa unaoharibu mila na silka za jamii. Usasa una faida nyingi kwa jamii. Usasa hukuza na kuendeleza utamaduni pamoja na kuzalisha maendeleo mbalimbali yanayohitajika. Walakini, unabagua mila silka na desturi za jadi na kuleta mambo ambayo ukiyafikiria hupati nafasi ya ubinaadamu. Hivyo, ni wazi kwamba, vipengele vya usasa vimeimarisha au kuzalisha mikengeuko mikubwa ya kitamaduni kutoka hali halisi ya maisha na mitindo ya maisha inayofaa kufuatwa na binaadamu. [1] anasisisitiza kuwa tafiti nyingi za Magharibi zimekuwa zikiangazia ustawi wa mila silka na desturi za kiijamii. Baada ya kugunduliwa kwa tatizo la kuendeleza tamaduni, Umoja wa Mataifa, kupitia mashirika yake, umeamua kuwa na kampeni maalumu za kulinda uasili wa chakula, hali ya hewa, mazingira, kupunguza umaskini, na elimu, ili kudhibiti madhara yanayoweza kujitokeza baadae.

### 3.2 Mivutano kuhusu Falsafa ya Kiafrika

Falsafa ni istilahi inayotumiwa kuelezea wazo au mawazo anayoyaamini mtu, mwandishi au mtunzi kuwa yale anayoyaandika, yana ukweli unaotawala misingi ya maisha. Kwa mtazamo wa mtaalamu huyu, falsafa ni imani na mawazo aliyonayo mtu juu ya jambo fulani kuwa na ukweli kulingana na maisha halisi ya jamii. Kwa ujumla falsafa ni itikadi au imani inayojenga misingi ya maisha ya taasisi za kisiasa, kijamii au kidini. Imani hizi hujengwa kwa mfumo wa fikra unaojaribu kueleza, kutafakari, na kuchambua mawazo, maadili, na mtazamo wa kidunia wa jamii za Kiafrika kuhusu maisha, ulimwengu, na nafasi ya binadamu ndani yake. Imani hizo, hulenga kutoa mwanga juu ya namna watu wa Afrika walivyokabiliana na masuala ya kimaadili, kijamii, kisiasa, kidini, na kisayansi katika muktadha wa tamaduni zao. Jamii za Waswahili nazo zimekuwa na imani za

kijamii juu ya mambo kadhaa. Filamu za *Matusi* na *Wali Wangu* zimesawiri vipengele mbalimbali vya falsafa.

### 3.2.1 Imani juu ya Mkole na Jando

Mtunzi wa filamu hizi ametumia mvutano wa kifalsafa ya Afrika ili kuibua thamani mahasusi kwa Waswahili. Mkole ni sehemu ambayo wanawake huwekwa kwa ajili ya kupewa mafunzo yanayohusu ndoa na maisha yake kwa ujumla. Mkole hutumika kama chuo kinachowaelekeza wanawake kujua tabia njema, kuheshimu wanaume na kuwa na kauli zenye tija kwa jamii. Mwanamke aliyefuzu mkoleni huwa na mbinu mbadala za kumtunza na kumuenzi mume, pamoja na kumtunzia heshima kila mtu. Mwanamke huyo huepukana na usungo. Pia, mkole huwa unafahamisha heshima na hadhi ya mwanamke aliye katika ndoa. Utafiti umebaini kuwa mvutano wa kimaadili una dhima ya kuonesha nafasi ya mkole kwa mwanamke wa Uswahilini kama chuo cha amali katika kuikabili ndoa yake. Hayo yanathibitishwa na mhusika Tifutifu pamoja na Chanuo wakati wakijadili suala hilo.

**Tifutifu:** Karibu kwangu
**Chanuo:** Unaishi wapi
**Tifutifu:** Nnaishi pale nimeolewa
**Chanuo**: Hongera kwa kuolewa
**Tifutifu:** Huku kwetu ndoa ni kipimo cha tabia njema, na kauli nzuri kwa wanawake, sio kwamba madunga embe hayapo.
**Chanuo:** Madunga embe ndio nini?
**Tifutifu:** Madunga embe ni wanawake wazuri
ambao wamekosa ndoa kwa sababu ya kauli au tabia chafu, kwani
wewe hukuambiwa mkoleni. Au mwezangu wewe mtu wa wapi?
**Chanzo**: *Matusi*, onesho la 9, dakika ya 8:18 hadi8:49

Tifutifu anaonesha thamani ya mkole katika kuijenga ndoa kwa kutofautisha wanawake walioolewa na wale madunga embe[2]. Pia, anaonesha kuwa mwanamke mwenye adabu ni lazima awe amefuzu mkoleni. Hivyo Waswahili wana imani juu ya mafunzo hayo.

Eneo jingine linaloonesha thamani ya mkole ni pale Tifutifu alipobainisha thamani ya mume kuwa haijulikani na mtu ambaye hajachezwa, yaani hajaenda mkoleni. Tifutifu anaonesha kuwa wanawake waliokosa kwenda mkoleni huwa wamekosa maarifa ya kuzitunza ndoa zao. Zaidi, anaonesha kuwa ndoa bora yenye thamani hujengwa mkoleni. Maneno hayo yanthibitishwa na mazungumzo yaliyofanywa kati ya Tifutifu na Chanuo katika onesho la kumi:

**Tifutifu:** Sasa utawezaje kujua thamani ya mume
nawe hujachezwa
**Chanuo:** Mambo hayo kule yanaonekanwa
Kama mambo yakishamba
**Tifutifu:** Ndio maana, niliwahi kusikia watu wa huko

[2] Kwa mujibu wa Makala hii, madunga embe imefasiriwa kama wanawake wanaosusa ndoa huku ukiwa wanaendeleza uasharati katika jamii.

mjini wanathamini sana CV kuliko vyeti, na ndi maana wanawake wanaolewa huko mjini ni wae waliotumika kingono na muowaji

**Chanzo**: (Matusi onesho la 10, dakika ya 1: 06 hadi 1: 39)

Nukuu hii inaonesha wazi kuwa wanawake waliotimiza maadili ya huwa na nafasi ya kwenda mkoleni. Kwa sababu nadharia ya Aksiolojia katika tawi la maadili inahimiza kukubalika kwa mila za jamii kama ilivyotokea kwa Tifutifu kukubali nafasi ya mkole. Aidha tawi la thamani linajitokeza pale walipojadili kwamba mtu hawezi kutambua thamani ya mume kama hajapata mafunzo ya mkoleni. Hivyo, ni wazi kuwa falsafa ya Waafrika kuhusu mafunzo hayo inajenga na kuimarisha ndoa.

Sehemu nyingine ambayo mkole unaonekanani jambo muhimu ni katika kustawisha maisha na uchumi wa wanandoa. Mafunzo ya mkoleni hayapo katika ushiriki wa tendo la ndoa tu, bali yapo kwa nia ya kuwafunda wanawake waweze kuwasaidia waume au katika kujiimarisha kiuchumi. Hali hiyo inathibitishwa na mazungumzo ya Tifutifu na chanuo. Wanasema:

**Tifutifu:** Kwa hali hiyo lazima asidumu ndoani, sisi tuliambiwa mkoleni wanawake wa aina hiyo lazima watafute wanaume wenye pesa, na wakiwafilisi tu wanaondoka.

**Chanuo:** Kwa nini?

**Tifutifu:** Kwa sababu hawana njia ya kumfanya wanaume afanikiwe. Wakati wanaume wakiungana na wake zao kufanikiwa, mwanamke wa aina hiyo hujipanga kimatumizi kwa lengo la kumfilisi mume. Tumeambiwa mkoleni kama pesa inaleta furaha kwenye maisha yetu basi hatuhitaji kuwa na mwanamme

**Chanuo:** Kumbe unahitaji nini?

**Tifutifu:** Kwa sababu kuolewa na mwanamme Tajiri ni ndoto ya kila mwanamke mvivu.

**Chanuo**: Kumbe huko mkoleni mnafundishwa mambo mengi eeh. Natamani nimuone huyo anayewafundisha huko mkoleni

**Tifutifu:** Kwani wewe hujafundwa? Sasa unaenda kufanya nini mbilini?

(**Chanzo**: *Matusi* onesho la 10, dakika ya 7:21 hadi8:04)

Maelezo hayo yanaonesha ubora na nafasi ya mkole kwa wanamke wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu mafunzo hayo yanatoa mwelekeo mzima wa namna ya kuishi na mume. Pia, yanaelekeza namna ya kupambana kiuchumi. Kuingia katika ndoa bila ya kuenda mkoleni inaaminiwa kuwa kuongeza mzigo wa familia tu na sio vinginevyo.

Kwa upande wake, filamu ya *Wali Wangu* inaonesha kuwa ndoa nyingi zinaaminika kuwa na vurugu kwa sababu wanawake wengi wamekosa kwenda mkoleni. Tusi kubwa linalotumiwa na msanii wakati wa kupatanisha ndoa ni usungo, likimaanisha mwanamke huyo hakupata maarifa mapana ya kuishi na mumewe. Sehemu ifuatayo ya filamu hii inathibitisha hili:

**Nyongo:** Sasa wewe ndio adabu gani hizo. Unashindwa kumpelekea mumeo maji bafuni. Hivi mimi ndugu yake ndio nimpelekee maji, wewe huoni kama hiyo si sawa au hujapata mafunzo ya kuingia katika ndoa mkoleni.

**Kidole:** Mambo ya ndoa yetu hayakuhusu.

**Nyogo:** Inaonekana hujafunzwa wewe na ndiyo maana msungo. Na siwezi kukulaumu kwa sababu umefata tabia za mama yako

**Kidole:** Msungo mwenyewe, tena sitaki kutajiwa habari za mama yangu kama wewe ni mwanamke na umefunzu mkoleni mbona bado upo kwenu hujaolewa. Msungo mwenyewe, mbwa wewe.

**Chanzo**: *Wali Wangu* onesho la 7, dakika ya 11:45 hadi 12: 06

Neno msungo linatumiwa sambamba na neno mkoleni kuashiria chuo wanachopaswa kwenda kila mwanamke wa Kiswahili ili ajifunze ujuzi wa kukaa na kumshughulikia mumewe. Taaluma hii inaonekana muhimu sana kwa sababu inaendelea kuhimizwa na viongozi wa dini. Kwa mfano, gazeti la *Mwananchi* (tarehe 16 /07/ 2022) linasema kuwa, hivi karibuni Zanzibar kumekuwa na nyuo vya ndoa ili kuwatayarisha wanaoingia katika ndoa maisha ya mume na mke. Mafunzo hayo ya ndoa yanagusa katika maeneo mbalimbali ya maisha ya wanandoa ili kuimarisha ndoa na kupunguza talaka. Ofisi ya Mufti Zanzibar inapaswa kupongezwa kwa kuunga mkono jitihada za taasisi mbalimbali katika kutoa elimu hii.

Mafunzo ya ndoa katika muktadha wa aksiolojia ya Kiafrika yanahusisha kuchunguza jinsi ndoa inavyothaminiwa na kueleweka ndani ya mifumo mbalimbali ya kitamaduni, kimaadili na kifalsafa. Aksiolojia, kama somo la maadili, hutoa nafasi ya kuchunguza thamani ya ndani na ya nje iliyotolewa katika ndoa katika jamii za Kiafrika. Mambo muhimu ya ndoa yanayohusiana moja kwa moja na Nadharia ya Aksiolojia ni pamoja na ujenzi bora wa taasisi ya kijamii. Ndoa za Waswahili hutazamwa kama taasisi muhimu ya kijamii katika tamaduni za Kiafrika kwa lengo la kujenga msingi wa utulivu wa familia na jamii. Ndoa za kitamaduni za Kiafrika huambatana na mila na desturi mbalimbali, kila moja ikibeba maadili muhimu ya kitamaduni. Mazoea haya yanasisitiza utakatifu na umuhimu wa ndoa. Tamaduni ya uchumba, ambapo familia ya bwana harusi hutoa zawadi kwa familia ya bibi harusi, ni jambo linalothaminiwa na jamii za Waswahili. Pia, itikeli, maadili na wajibu wa kijamii nao unahusishwa moja kwa moja na aksilojia katika ndoa. Katika ndoa za Waswahili, wajibu na matarajio ya kijamii katika kujikamilisha kuwa mume, baba na mama.

Kamage (ht) anaeleza kuwa, jamii za Kiafrika huchukua hadhari kubwa katika sekta ya ndoa kuhusu maadili. Anamaanisha kwamba; ndoa familia na unyumba ni vitu visivyochezewa. Kusudi la ndoa ni kuendeleza nguvu-uhai kupitia uzazi wa watoto. Hivyo, ili kujenga ukoo mzuri ni lazima kuzingatia masuala ya maadili. Ndoa ni daraja linalounganisha mnyororo wa nguvu-uhai. Walio hai na wafu huunganishwa na kuwa pamoja. Kizazi kilichopita kinawakilishwa na wazazi; kilichopo kinawakilishwa na maisha ya mtu anayoishi na kijacho kinaletwa kupitia uzazi wa watoto. Kwa njia hii, ndiyo maana maadili huzingatiwa.

### 3.2.2 Nafasi ya Uzazi na Malezi ya Watoto

Katika jamii za Waswahili, suala la kuwa na mtoto au uwezo wa kuzaa na kuzalisha linatazamwa kwa thamani kubwa. Ni miongoni mwa itikadi zinazoaminiwa na jamii kuwa ndio utajiri au baraka. [6] anaunga mkono hoja ya kwamba, Waafrika huthamini sana watoto. Anaongeza kuwa, thamani ya mwanamke wa Kiafrika hupatikana kutokana na kuwa na uwezo wa kuzaa watoto wengi. Kutoweza kuwa na watoto huchukuliwa kuwa ni balaa na nuhusi. Hii ni kwa sababu watoto huchukuliwa kuwa baraka katika ndoa na jamii kwa jumla. Naye Faustine [5] anamwelezea mtu mwenye uzazi kutazamwa kama mtu mwenye baraka nyingi zinazotokana na kuwapo kwa nguvu-hai. Hii ni kwa sababu Waafrika wanautazama uzazi kama njia ya kuwapo kwa mtu na njia pekee ya kuukuza na kuuendeleza ukoo. Hali hii haitazamwi kwa mwanamke bali hata kwa mwanamme.

Katika filamu ya *Wali Wangu,* swala la uzazi linatazamwa jambo la kuondosha aibu na kuipa furaha familia. Kufanya tendo la ndoa na kubarikiwa mtoto kunaonekana kuwa na tija kwa familia na taifa kwa ujumla. Hayo yanathibitishwa na Katambuka katika mazungumzo yake. Anasema:

> **Katambuga**: Kumbe ilichafuka, nimeitafuta ndani
> bila mafanikio, ndio nakuja kukuuliza.
> **Sulupu**: Nguo inanuka mikojo, unaivaa uende nayo wapi?
> **Katambuga**: Kumbe niliikojolea, aayaa! Kitu
> ambacho sikipendi kuwa kikojozi
> **Sulupu**: Usijali, pengine ndio njia ya kuiondoa pombe.
> **Katambuga**: Mimi sitaki kuondoa pombe katika hali
> ya kikojozi, Mimi nataka kuwa mkojoaji,
> maana nikiwa mkojoaji nitaleta tija kitaifa, ukiwa kikojozi unaleta
> aibu kifamilia
> (**Chanzo**: *Wali Wangu,* onesho la 1, dakika ya 16:14 hadi 16:51)

Katika mazungumzo haya, tunaona jinsi Waafrika wanavyothamini na kuipa nafasi kubwa jamii inayoundwa na watoto. Katambuga anaeleza kwa njia ya kinaya umuhimu wa kuwa na uwezo wa kuzaa "kuwa mkojoaji" na kuchangia ukuaji wa jamii kwa kuleta watoto. Hii inaashiria imani ya Waafrika kwamba mtoto ni sehemu muhimu ya jamii na urithi wa kifamilia.

Pia, Katambuga anapingana na dhana ya kuwa "kikojozi" mtu ambaye hana tija au faida kijamii; kinyume chake anapenda kuwa na nafasi ya kuwa "mkojoaji," ambaye ataleta manufaa kwa jamii kupitia uzazi. Mazungumzo haya yanaonyesha jinsi uzazi unavyochukuliwa kama jukumu la kijamii ambalo lina heshima na lina mchango katika kuimarisha familia na jamii kwa ujumla.

Eneo jengine ambalo wanaume wanajifaharisha nalo ni kuweza kufanya tendo la ndoa. Huwa fahari ikiwa mume huyo anaweza kupata mtoto kupitia tendo hilo. Aidha, kupitia mila na silka za Waswahili, tendo la ndoa halitazamwi kama ni starehe tu, bali njia ya kufanya maombi kwa muumba ili kupata mtoto. Maelezo hayo yanathibitishwa na kauli za Katambuga. Anasema

> **Katambuga:** … Sasa mimi nataka nikamtumie

mkewe wangu saa hizi, kwa sababu pombe zishashuka. Nataka nikapeleke maombi ya uumbaji wa mtoto kwa mungu, wewe sulupu twende huku.

**Chanzo**: *Wali Wangu,* onesho la 1, dakika ya 12:15 hadi 12:25

Katika mazungumzo haya, Katambuga anadhihirisha kwamba, tendo la ndoa lina maana kubwa zaidi kuliko starehe tu, linaweza kuwa njia ya kuomba na kutafuta mtoto kutoka kwa Mungu. Katambuga anapotaja "maombi ya uumbaji wa mtoto," anasisitiza umuhimu wa uzazi katika ndoa na heshima ya kiroho inayohusishwa na mchakato huo.

Mazungumzo haya yanaonesha kwamba, tendo hilo linapaswa kuwa na lengo la pamoja kati ya wapenzi. Hii inaonesha kwamba, katika tamaduni nyingi za Kiafrika, tendo la ndoa linaweza kutazamwa kama sehemu ya mchakato wa kuleta watoto, na hivyo kuwa na lengo la kiroho zaidi, huku likionesha umoja wa familia na dhamira ya kuendelea na kizazi. Kwa hivyo, Katambuga anaunda picha ya tendo la ndoa kama hatua muhimu katika maisha ya kifamilia. Hatua hiyo, inahusisha imani na matakwa ya kiroho ya kupata watoto. Ushahidi mwingine unaonesha nafasi ya mtoto katika jamii ya Waswahili ni maelezo ya Katambuga. Anasema:

**Mwahija**: Katambuga naona kichwa kimekaa pahala pake?
**Katambuga** (*akipepesuka kwa ulevi*) unamaanisha kichwa gani
**Mwahija:** si hicho chenye ubongo.
**Katambuga:** Vichwa vya wanaume vyote vinaubongo,

ila hiki kimoja ubongo ukimwagika sehemu sahihi huleta manufaa kitaifa na huumbamwili mwingine

**Chanzo**: *Wali Wangu,* onesho la 1, dakika ya 5:51 hadi 6:8

Katika mazungumzo haya, Katambuga anatoa mfano wa maana ya "kichwa chenye ubongo" kwa njia ya Kimajazi na kinaya. Hii inaonesha wazi kuwa maadili ya jamii yalizingatiwa katika mazungumzo hayo. Ubongo huo maana yake mbegu za uzazi na hatua ya kuleta watoto. Katambuga anaposema "ubongo ukimwagika sehemu sahihi huleta manufaa kitaifa na huumba mwili mwingine" anaigusa moja kwa moja nadharia ya Aksiolojia kupitia msingi wake unaosema Uzuri wa fasihi unaweza kujitokeza katika matumizi ya lugha ya kisanii. Kanuni hii inasisitiza umuhimu wa lugha, taswira, na mtindo katika kujenga tajriba ya kusoma yenye maana na ya kufurahisha. Maelezo hayo yalikuwa yamejaa *Matusi* lakini kwa namna yalivyoelezwa unaifanya filamu hii kuwa na maadili ya jamii. Anasisitiza kwamba tendo la kuzaa si suala la kibinafsi tu, bali ni jambo la manufaa ya kijamii na hata kitaifa. Kwa mtazamo wa aksiolojia, thamani ya tendo la kuzaa katika jamii za Kiafrika hupatikana kutokana na mchango wake katika kuendeleza jamii kwa njia ya urithi na kuimarisha kizazi kijacho. Watoto, katika muktadha huu, wanachukuliwa kama baraka na hazina muhimu kwa jamii.

Kwa vile Nadharia ya Aksiolojia inafafanua thamani inayoamini wa na jamii, tunaweza kuona kwamba kuzaa watoto kuna thamani ya juu katika imani ya Waafrika. Tendo la ndoa halitumiki

kwa kuridhisha matakwa binafsi tu, bali kwa kuendelea kuzalisha kizazi kipya na kulinda urithi wa jamii. Mazungumzo haya yanaonesha jinsi watoto wanavyothaminiwa kama sehemu ya utajiri wa kijamii. Umuhimu wa uzazi unaonekana kama mchakato wa kutoa mchango wa maana katika jamii kwa namna ya kiroho na kiutamaduni.

Kwa upande wa filamu ya *Wali Wangu*, mtoto amepewa nafasi ya kutunza na kuimarisha ndoa. Katika onesho la 9, mwanamke anaomba kufanya tendo na mfanyakazi wake wa ndani ili aweze kupata mtoto kwa ajili ya kuimarisha na ndoa yake. Wakati mhusika Kambaulaya anafukuzwa na bosi wake kwa tuhuma ya uchawi, mama mwenye nyumba anatetea kubaki kwa mhusika Kambaulaya. Hii ni kwa sababu ndiye aliyezaa naye watoto wawili ambao mume wa ndoa anajivunia kuwa watoto wake. Hivyo, ndiye anayeimarisha ndoa yake. Hayo yanaonekana katika dayalojia hii:

**Kambaulaya**: Bosi eshasema mimi niondoke ntafanya nini, kama kumshawishi nibaki ni wewe unayelala kitanda kimoja ndio ungeweza.

**Mke wa mandozi**: Unaondokaje, wakati wewe ndio uliyeifanya ndoa yangu kuwa na furaha?

**Kambaulaya:** Mimi nilipanda mbegu kwenye shamba la watu na wewe ndio ulinishawishi kufanya hivyo kwa ajili ya kulinda ndoa yako.

**Mke wa Mandozi**: Yaani hufikiri kabisa kuhusu hii mimba wakati wewe ndio mwenye uhalali kabisa.

**Chanzo**: *Matusi* onesho la 9, dakika ya 4:6 hadi 4:25

Maelezo hayo yanaonesha namna anavyojilaumu kwa kuzini na mke wa mtu, kitendo ambacho ni kinyume na maadili. Hivyo, msimbo wa kimaadili unaozungumzia jambo zuri ni lile linalokubaliwa na jamii linaonesha kukosekana kwa maadili ya Kambaulaya na Mke wa Mandoza. Hata hivyo, jambo hilo lilifanywa kwa sababu ya kuimarisha ndoa ambayo ilishaanza kulegalega na kutaka kuvunjika. Ndoa hiyo ilitaka kuvunjika kwa sababu mwanamke hashiki mimba, ilhali tatizo hilo lilikuwa la mume. Hali hiyo inaonesha wazi namna mimba inavyothaminiwa. Hii ni kwa sababu baada ya mke kuwa na mimba na kupata mtoto ndoa hiyo ilizidi kuimarika na kuwa na mapenzi. Nadharia ya Aksiolojia kupitia fikra inayosisitiza kuwa kitu kizuri ni kile kinachothaminishwa kupitia idili za jamii inaonesha kuwa mimba na mtoto ni sehemu ya idili za kijamii. Hivyo ni wazi kuwa mtoto katika jamii ya Waswahili huhesabiwa kama ishara wa uimara wa ndoa.

Fahari ya mzazi kwa a watoto wake ni eneo jingine linaloonesha nafasi ya mtoto katika jamii za Waswahili. Mzazi kujifaharisha kwenye utii wa mtoto huyo. Waswahili huona fahari pindi mtoto anapokuwa na utiifu mbele ya wazazi wake au wakubwa wake. Mtoto anachukuliwa kuwa mdogo mbele ya wazazi wake hata awe na umri mkubwa i. Hivyo anapaswa kuwa, mtiifu na mwenye kutekeleza yale wasemayo wazazi wake. Ikiwa itatokea anataka kupingana na jambo hilo, anapaswa kulisema kwa ushauri au kwa mtindo wa ombi. Wakati huohuo mzazi ana nafasi ya kutoa amri kwa jambo lolote mbele ya mwanawe. Hayo yanathibitika katia maelezo yafuatayo:

**Kutafuna:** Hayo ndio maamuzi ambayo mimi nimeyachukua dhidi ya mwanamke wako.

**Bashite:** Sawa, nakuelewa mjomba, lakini inahitaji muda ili niweze kukubaliana na hicho unachokitaka.

**Kutafuna:** Aaaa hapana cha muda hapo, hakuna cha muda hapo. Mimi natumia mamlaka nikiwa kama mzazi. Mwanamke wako lazima afunde ili akatoe funzo kwa wanawake wengine huko mjini.

**Bashite:** Umeshaangalia athari itakayotokea.

**Kutafuna:** Ndio, kwa sababu nisipomfundisha kama mzazi nitateketeza famiilia, pia natakiwa niende na majibu mbinguni.

(**Chanzo**: *Matusi* onesho la 1, dakika ya 21:12 hadi 21: 23)

Nukuu hii inaonesha kuwa mzazi ndiye mwenye amri ya mwisho dhidi ya mtoto wake. Amri hiyo huwa inalenga kumlea. Mtoto wa Kiafrika anakabiliwa na kaida maalumu anazopaswa kuwa nazo mbele ya mzazi wake. Mtoto huyu huwa na uhuru wenye mipaka na nidhamu maalumu. Katika sehemu ya malezi, mzazi anatazamiwa kubeba jukumu kumbwa kwa mwanawe. Mzazi ni masuulu wa kila hatua ya malezi, kiimani na kimila. Hivyo, mzazi yeyote huwa anafanywa hayo si kwa lengo la kuthibiti uhuru bali falsafa ya Kiafrika ndivyo inavyoamuru. Nukuu nyingine inayoonesha malezi kwa mzazi inajitokeza kwenye mazungumzo yafuatayo:

**Bashite:** Nisamehe mjomba, ila sikujua kama haya yanaweza kutokea

**Kutafuna**: Sawa, ila sikuruhusu uondoke hadi ujifunze athari ya misungo inayotoka mjini.

**Chanzo**: *Matusi,* onesho la kwanza, dakika ya 16:54 hadi 17:03

Nukuu hii inapewa msisitizo na Kutafuna anapohimiza kuwa, mchumba wa Mswahili lazima apate wazee wenye ujuzi wamfunde kabla kuingia kwenye ndoa. Anasema:

**Chanuo:** … Kwa hiyo sisi wengine hatuna haki ya kuolewa?

**Kutafuna:** Mnayo haki ya kuolewa, lakini lazima ufundwe na kungwi atakaye wafundisha jinsia yenu, kufunwa na mitandao haikufanyi kuwa mke thabiti mbele ya mke bora.

**Chanzo**: *Matusi*, onesho la 1 dakika ya 32:3 hadi

Malezi kwa mtoto hayakuishia katika hali ya umri mdogo tu, bali wazazi wanamchukulia mtoto wa Kiafrika ana haki ya kupatiwa malezi na mafunzo hadi yanayomuimarisha katika ndoa yake. Mzazi ndiye anayebeba jukumu la kuona ndoa ya kila mtoto inastawi. Fuluge **[6]** anaona kuwa, asasi ya ndoa ndiyo humpa mwanamke jukumu la kuzaa, kuhudumia familia na kumtunza mume pamoja na uangalifu wa nyumba yake. Hali hii inarudi kwenye jukumu la msingi la wazazi, ambalo ni kuzaa na kulea. Pia, Faustine (2017) anamwelezea mtu mwenye uzazi kutazamwa kama mtu mwenye kuheshimika kutokana na baraka aliyojaaliwa na Mungu. Baraka hizo zinatokana na kuwapo kwa

nguvu-hai iliyomo ndani ya miili ya watu waliofikia baleghe. Hali hiyo inawaandaa Waafrika kuutazama uzazi kama njia ya kuwapo kwa mtu na njia pekee ya kuukuza na kuuendeleza ukoo. Hivyo, mtu mwenye uzazi hupewa heshima kuliko yule asiye na uwezo wa kuzaa.

### 3.2.3 Imani kuhusu Kifo

Imani kuhusu kifo ni moja ya falsafa ya Kiafrika, ambayo mtuzi wa filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu* ameona kuna sababu ya kuifafanua kwa kuwa miongoni mwa sababu za mivutano ya kimaadili. Dhana ya kifo imewekwa bayana kupitia mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule unaoegemea kwenye sayansi ambao unajikita katika kuonesha ukomo wa viungo vya mwanadamu katika kufanya kazi. Pili, ni mtazamo wa kifalsafa unaojikita katika kuimulika mitazamo ya mwanadamu katika kuifafanua dhana ya kifo. Mitazamo hiyo imebeba ukweli wa jamii husika unaoaminiwa na kuzingatiwa katika kuifikia hatima yao (kifo) kwa kujiegemeza katika mila na desturi zao. Kwa Waafrika, kifo ni tukio linaloibua simanzi kubwa kwa wanajamii, na linapotokea huomboleza kwa kujiegemeza katika misingi ya dini aliyojikita nayo marehemu katika jamii yake.

Ukweli huu ndio unaojitokeza katika filamu ya *Matusi*, katika filamu hii kifo kinatazamwa kama mpango wa Mungu. Hivyo, maiti anapaswa kuheshimiwa na kila mtu. Kwa sababu inaaminiwa kuwa, mwili huacha dunia na roho huwa hai na huwatembelea wale waliopo duniani kila baada ya muda .

> **Kashuba:** Tumesema hazikwi mtu hapa, mnawezaje kumzika huyu kama mmezaa peke yenu.
>
> **Kutafuna**: …hapa kumbuka kifo ni mpango wa mungu baada ya binaadamu kumaliza kazi yake. Lakini mazishi ni mpango wa binaadamu wa kutayarisha mwili huo na kuupeleka kwa Mungu
>
> **Chanzo**: *Matusi* onesho la kumi na tatu (13) dakika ya 16: 15 hadi 16:37)

Kwa ujumla, nukuu hii inafafanua kuwa, imani za Waafrika kuhusu kifo ni mchanganyiko wa mambo mawili muhimu, kifo ni mapenzi ya Mungu na mazishi ni jukumu la kijamii. Wanafikiri kwamba, kifo ni sehemu ya mpango wa Mungu. Wakati mtu anapokufa, jamii ina jukumu la kumheshimu kwa kufuata taratibu za mazishi, ambazo pia ni sehemu ya mipango ya kitamaduni. Kutafuna anaendelea kusema kwamba "mazishi ni mpango wa binaadamu wa kutayarisha mwili huo na kuupeleka kwa Mungu." Hii inaonesha kwamba, ingawa kifo ni mapenzi ya Mungu, mazishi ni jambo linalofanywa na wanadamu. Mazishi ni mchakato wa kijamii na kitamaduni ambapo jamii huungana kutunza na kuandaa mwili wa marehemu kwa ajili ya safari ya mwisho. Wakati wa mazishi, watu wanakutana kumheshimu marehemu na kumkabidhi kwa Mungu. Inadhihirisha kwamba, kifo kinasimamiwa na Mungu, lakini wanadamu wana jukumu la kutoa heshima na kufanya taratibu za mazishi.

Kwa vile Waswahili wanazo imani za dini, mtazamo huu umeathiriwa mno na dini ya Uislamu na Ukristo. Ushahidi wa haya ni Qur'an 3:145 (Sura ya Al-Imran), ambayo inasema: "Na hapana atakayekufa, isipokuwa kwa idhini ya Allah, kwa muda ulioainishwa. Na atakayehitajika malipo ya

dunia, atalipwa, na atakayehitaji malipo ya Akhera, tutamlipwa. Na sisi ni wenye kudhibiti." (Qur'an 3:145). Pia, kwa upande wa Biblia, Warumi 14:8 inasema: "Kwa maana, ikiwa tunakufa, tunakufa kwa Bwana; na ikiwa tunaishi, tunaishi kwa Bwana. Hata hivyo, iwe tunakufa au tunaishi, sisi ni wa Bwana." Aya hii inasisitiza kwamba, kifo kimo katika mipango ya Mungu na kinatokea tu kwa idhini yake na kwa wakati maalumu alioandaa. Hivyo, kifo ni sehemu ya mapenzi ya Mungu, na hakuna anayeweza kufa kabla ya muda wake ulioainishwa na Mungu.

Eneo jingine linaloonesha kuwa kifo ni miongoni mwa imani thabiti ya Afrika ni kutukuza imani juu ya roho iliyokufa kuwa hai na kuwatembelea wanadamu duniani. Roho hiyo inaaminika kuwa, inaweza kusababisha madhara au manufaa kwa jamii.

**Chanuo:** Huyo mjomba wako ana maneno ya kichawi

sana huyu? Eti anasema mtu hawezi kutoroka na

akitoroka atapata ajali au kufa kutokana na kuzindikwa kijiji hiki na wazee waliokufa

**Bashite:** Kwani wewe ulitaka kutoroka?

**Chanzo**: *Matusi* onesho la pili dakika 1:10 hadi 1:37

Nukuu hii inathibitisha imani kwamba roho za wafu zinahusiana na jamii na zinaendelea kuwa na athari kwa wale walioko hai. Roho za wafu, kama ilivyoonyeshwa na wazee waliokufa kwenye kijiji, ni sehemu ya mifumo ya kijamii na, mara nyingi, hutumika kudumisha sheria, maadili, na kanuni katika jamii. Sentensi inayosema mtu atakayejaribu kutoroka kutoka kijijini anapaswa kuwa na tahadhari, kwani kuna uwezekano wa kupata ajali au kufa kutokana na "kuzindikwa kijiji hiki na wazee waliokufa" inaonyesha imani kwamba roho za wazee waliokufa zinakaa katika kijiji na zinaweza kuathiri maisha ya wale wanaoishi. Katika jamii nyingi za Kiafrika, kuna imani kwamba roho za wafu zinatayarisha mazingira ya jamii, zikiwatunza na kuwapa Baraka. Akishadidia maelezo hayo, Madebe (2023) [3]. Anasema;

> Waafrika tunapata shida ya maisha. Ukiwa duniani harakati za maisha zinakupiga. Lakini hata ukifa haina maana kuwa utapumzika. Hapo ndugu zao hukutwisha mzigo wa kutatua matatizo yao, maana kabri lako huligeuza kuwa mzimu na kuelekeza maombi kwako.

Kwa upande wa *Wali Wangu*, wafu walitukuza kwa kuendeleza mambo waliyoyaacha. Utekelezaji huo ndio ulioaminika kuwa baraka kwa jamii kama inavyosawiriwa katika dayalojia ifuatayo:

**Batani:** Nimesikia kilichojiri jana, lakini haya sio

mageni ulishawahi kuyashuhudia kwa babu yako.

[3] Maelezo hayo yalitolewa na Madebe Lidai wakati wa mahaojiano na chanali ya mtandaoni ya Wasafi medium. Madebe ni mtuzi wa filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu.* Pia, ameshiriki katika kuigiza na kuongoza filamu hizo. Chaneli hiyo imetazamwa na mtafiti tarehe 20/11/204.

**Mwalimu** Ni kweli kabisa haya hayanikatishi tamaa kwa sababu nimeachiwa mikoba na babu yangu. Ili nikiendeleze hiki kizazi. Batani unajua kwa nini kipindi cha uhawara mnadumu sana.

**Batani:** Sijui

**Mwalimu**: Haya aliyatabiri babu yangu wakati yupo mahututi na ndiyo maana akanikabidhi hii kazi. Na mimi nipo ili kubeba waraka wa babu yangu ili niokowe kizazi.

**Chanzo**: *Wali Wangu,* onesho la 2, dakika ya 21:3 hadi 22:14

Maelezo haya yanaonesha wazi kuwa, waliokufa wamepewa daraja la heshima kwa jamii. Kwani inaaminika kutekeleza mikoba au mila za waliokufa ni kupata baraka katika maisha. Neno waraka ndio linalowakilisha mikoba ya marehemu. Hata hivyo, kifo kinazua mijadala mingi kwenye jamii. Wapo wanaoamini kifo hutokana na maradhi, kurogwa au nguvu ya mungu. Pia, kuna madai ya kuwapo kwa vifo vinavyosababishwa na usihiri kama asemavyo **[2].** Anasema:

> *Most societies in West Africa believe that death cannot be controlled and would take anyone irrespective of position, (age), sex or race, West African traditional believers have a firm belief that only the aged should die; the death of a young man therefore is attributed to some supernatural forces.*
>
> Jamii nyingi za Afrika Magharibi zinaamini kuwa kifo hakiwezi kudhibitiwa na kinachukua mtu yeyote bila kujali nafasi, umri, jinsia au rangi. Waumini wa dini za jadi za Afrika Magharibi wana imani thabiti kwamba ni wazee pekee ndio wanapaswa kufa; kifo cha kijana kinahusishwa na nguvu za kishetani (tafsiri yangu)

Maelezo haya, yanaonesha kwamba katika jamii nyingi za Afrika Magharibi, kifo hakidhibitiwi na binadamu. Hii ina maana kwamba kifo ni tukio linalotokea kwa mapenzi ya nguvu za kiroho au kimungu, na hakuna mtu anayeweza kukiepuka au kulikwepa, bila kujali nafasi yake, umri, jinsia, au rangi. Katika imani hii ni ukweli kwamba kifo ni sehemu ya mpango wa asili wa ulimwengu na hutokea bila kujali hadhi ya mtu au mazingira yake. Hii inaonyesha kwamba kifo kinachukuliwa kama tukio lisilotabirika na linaloshikiliwa na nguvu za juu ambazo ziko nje ya uwezo wa mwanadamu.

## 4.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Thamani ya fasihi hupimwa kwa mujibu wa manufaa wanayoipata wanajamii walioandikiwa fasihi hiyo. Waswahili nao wanategemea thamani kutoka katika fasihi yao. Hivyo, filamu ya *Matusi* na *Wali Wangu* imegusa moja kwa moja mahitaji ya Waswahili kwa kufafanua mila na silka za Waswahili. Hivyo basi, watunzi wa filamu wanapaswa kuzingatia maadili ya jamii ili fasihi zao ziwe zao la jamii na sio kuhawilisha filamu za ulaya na kuzifanya za Waswahili. Kufanya hivyo kutastawisha fasihi yetu na tutanufaika na taaluma zilizopo katika jamii yetu. Aidha, matumizi ya nadhaaria zenye mrego wa kukubaliana na maadili ya kiafrika zinapaswa kutumika katika filamu za

kiswahili. Vilevile, watunzi wa filamu wanapaswa kuwa wabunifuna wenye kueleza uhalisia wa maisha au tukio linaloeleza ukweli wa maisha ya waswahili na Waafrika kwa ujumla.

**MAREJELEO**

**[1.]** Ackah, K. (2014). Antiquity versus modernity: Aspects of lifestyles and life-conditions. *Katika Legon Journal of the Humanities, 25*. Department of Philosophy and Classics, University of Ghana, Legon

**[2]** Amponsah, K. (1975). *Topics on West African traditional religion*. Religious Studies, 2. New York: oxford Publisher.

[3] Chairina, I. A. (2019). An analysis of moral values in the movie *COCO*. In *Proceedings of the 2nd English Education International Conference (EEIC) in conjunction with the 9th Annual International Conference (AIC)* (p. 62). Universitas Syiah Kuala, Banda Aceh, Indonesia.

[4] Davies, D. (2007). *Aesthetics and literature*. London: Oxford University Press.

**[5]** Faustine, S. (2019). Falsafa ya Waafrika kama kijenzi cha mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya za Kiswahili. In A. S. Ponera & Z. A. Badru (Eds.), *Koja la taaluma za insia: Kwa heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.

**[6]** Fuluge, A. (2021). Usawiri wa mchakato wa kujiua katika riwaya za Euphrase Kezilahabi: Ni mwangwi wa mtanziko wa kijamii? Unpublished master's thesis, Chuo Kikuu cha Dodoma.

**[7]** Lamarque, P. (2008). Aesthetics and literature: A problematic relation? *Philosophical Studies, 135*(1), 85.

**[8]** Mosweunyane, D. (2013). The African educational evolution: From traditional training to formal education. *Higher Education Studies, 3*(4). https://doi.org/10.5539/hes.v3n4p50

**[9]** Sanga, N. A. (2021). Thamani ya ujumi wa Kiafrika katika hadithi fupi *Simulizi za Kiswahili*. *MULIKA, 40*(1), 114.

**[10]** Stecker, R. (2019). Two definitions of artistic value. Central Michigan University.